




Mama Koki amekuwa
akichuma kabeji wiki nzima.
Dona, Maya na Duki
humsaidia Mama Koki
katika bustani yake kila
Jumamosi asubuhi. Leo
watoto hawa watahesabu na
kupakia kabeji. Baba Koki
atayapeleka masanduku
yaliyojaa kabeji sokoni
kuuza.




Teksi iliwafikisha watoto kwenye lango la bustani. Waliliona rundo kubwa la kabeji karibu na gari la Baba Koki. "Salala! Kabeji nyingi kweli!" Maya alishangaa. "Bila shaka kuna kabeji elfu moja hapo!" Duki alicheka. "La! Hasha! Pengine ni mia mbili tu!" Dona alipinga.



6

Mama Koki alikuwa amewasubiri langoni. "Hamjambo, nimefurahi kuwaona!" Aliwasalimu watoto. "Hebu tuanze kazi. Mtahesabu na kuweka kabeji kumi na mbili katika kila sanduku. Nina masanduku 20. Wawili kati yenu watapakia kwenye masanduku 7 kila mmoja. Aliyebaki, atapakia kwenye masanduku 6."



Watoto walilitazama lile rundo la kabeji. Wakajadili njia tofauti za kuzihesabu kabeji hizo. "Mimi nitahesabu zangu mbili mbili," Maya akasema. "Ninapenda kuhesabu nne nne. Ni haraka," Duki akajibu. "Mimi nitazihesabu tatu tatu ili niwe tofauti nanyi!" Dona akawajibu.



Watoto walijaza masanduku yote 20. "Kazi nzuri!" Mama Koki aliwapongeza.
"Tazama, kabeji zimezalia. Nguruwe wangu wanazipenda. Hebu tuwagawie," Mama Koki aliamua. "Mlipakia jumla ya kabeji ngapi katika masanduku yote? Ni kabeji ngapi zilizalia?" aliwauliza watoto.



Waliandika bei kwenye kila sanduku. Halafu, wakamsaidia Baba Koki kuyapakia kwenye gari. Waliweka nusu ya masanduku upande mmoja. Na nusu nyingine upande wa pili ili uzito ulingane.



"Karibu tukamilishe kazi!"
Baba Koki alisema. "Hebu
tuone ni masanduku
mangapi tunahitaji kuweka
kila upande."



Muda mfupi baadaye,
masanduku yote 20
yalikuwa yamepakiwa
kwenye gari. Baba Koki
aliondoka kwenda sokoni.
Aliwaza, "Nikifaulu kuuza
masanduku yote, nitapata
pesa za kutosha. Nitaweza
kuwashangaza watoto kwa
kurekebisha zizi la
nguruwe!"




Nyumbani, Mama Koki na watoto walinyunyizia mimea maji na kukusanya majani. Kufikia saa sita, wote walikuwa wamechoka. Mama Koki aliwaambia, "Ni wakati wa karamu yenu. Je, mnajua nilichowaandalia leo?"



Aliingia ndani kuwaletea
alichokuwa amewaandalia.
Watoto walisubiri kwa
uvumilivu huku wakikisia
atakacholeta. Aliporejea,
waliona mifuko ya kimori
chake ikiwa imeja!




"Hebu tuone ikiwa mlikisia sawa! Nimewatayarishia nini leo?" Mama Koki aliyaweka matofaa mezani. "Nilikisia sawa!" Duki alisema kwa furaha. Mama Koki aliwaambia watoto, "Kumbukeni sharti! Gawanya sawa ili kila mmoja apate haki yake. Hakuna anayepata zaidi wala kidogo kuliko mwingine!"



Kwanza, watoto walihesabu
matofaa mawili mawili.
Walihesabu: 2, 4, 6, 8, 10, 12,
14, 16, na tofaa moja
likabaki. Yote pamoja,
yalikuwa matofaa 17.



Waligawana matofaa
sawasawa yakabaki matofaa
mawili. Kisha watoto
waliyaweka matofaa yao
mikobani ili waende nayo
nyumbani kwao.



"Hebu tuyakate matofaa mawili yaliyobaki ili tugawane kati yetu," Duki aliwaambia. "Kila mmoja wetu atapata vipande vingapi vyatofaa?" Maya aliuliza. "Ninajua jibu!" Dona alitabasamu.



Wakati huo, Baba Koki alirejea nyumbani kutoka sokoni. Gari lilikuwa tupu naye aliquwa akitabasamu. "Niliuza kabeji zote. Sasa ninaweza kurekebisha zizi la nguruwe. Nitaweza pia kuwanunulia ule mpira wa miguu mliotaka." Watoto walishangilia, "Yee!"

